

Maswali

1. Zakayo aliishi wapi?
2. Zakayo alifanya kazi gani?
3. Je! Utajiri wa Zakayo ulimpa furaha?
4. Nani alikuja Yeriko?
5. Nani alitaka kumwona Yesu?
6. Mbona Zakayo hakuweza kumwona Yesu?
7. Alifanya nini?
8. Yesu alifanya nini alipofika kwa mkuyu?
9. Zakayo aliamua afanye nini?
10. Alijisikiaje alipoambia Yesu atakachofanya?

Majibu

1. Zakayo aliishi Yeriko.
2. Alikuwa mtoza ushuru.
3. La hasha. Alikuwa na huzuni na upweke.
4. Yesu alikuja Yeriko.
5. Zakayo alitaka kumwona Yesu.
6. Zakayo alikuwa mtu mfupi. Hakumwona kwa ajili ya umati.
7. Alipanda juu ya mkuyu kumwona Yesu.
8. Yesu alimwambia Zakayo ashuke chini. Alienda kwa nyumba ya Zakayo.
9. Zakayo aliamua kurudisha pesa alizopata kwa udanganyifu na kupeana nusu ya utajiri wake kwa maskini.
10. Alikuwa na furaha.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 1 Mwaka wa 1

42 Zakayo

Marejeo

Luka 19:1-10

Kiini cha somo

Kuonyesha vile upendo wa Yesu ulimbadilisha mtu aliyekuwa na upweke.

Maneno maalum

1. Yeriko + Zakayo + upweke + tosha kodi (ushuru) + Yesu.
2. Yesu akaja + mtu mfupi + umati.
3. Mkuyu + panda juu + weza kuona.
4. Yesu + uso mzuri + angalia juu + Zakayo shuka + nyumba yako.
5. Zakayo + wasiwasi + mnyang'anyi + danganya + rekebisha + lipa + furaha.

42.1 Yesu na wanafunzi walikuwa wanatembea katika mji wa Yeriko. Na siku hiyo watu walikuwa wamekusanyika katika mji wa Yeriko. Na hapo aliishi mtu mmoja aliyeitwa Zakayo. Ingawaje Zakayo alikuwa ni tajiri sana hata hivyo alikuwa ni mpweke na asiye kuwa na furaha. Wakati huo Wayahudi hawakuwa na mfalme wao wenyewe ambaye ni mwisraeli kwa maana nchi yao ilikuwa ikitawaliwa na Utawala mkuu wa Rumi katika nchi yao. Na watu walitakiwa walipe fedha, ambayo iliitwa kodi kwa mtawala.

Na katika kila mji alikuwepo mtu ambaye alikuwa akikusanya fedha hii kwa utawala wa Rumi. Zakayo ndiye mtu aliyekusanya fedha ya kodi katika mji wa Yeriko. Na hii ndiye sababu hakuna mtu aliyekuwa anampenda. Hawakupenda kulipa kodi kwake. Na mara nyingi alidanganya watu hata akawasababisha kulipa ushuru mkubwa sana. Kulikuwa na kitu ambacho Zakayo alikitamani sana kuliko kitu chochote. Alitaka kumwona Yesu. Alikuwa amesikia mengi sana kuhusu Yesu, kuhusu miujiza aliyoifanya, uponyaji na upendo wake kwa kutendea mema maskini na waliokuwa na upweke. Mara nyingi alifikiria ni jinsi gani ataweza kumwona Yesu siku moja na kuongea naye.

42.2 Alikuwa hajawahi kumwona Yesu, kwa hiyo unaweza kuwa na uhakika na furaha aliyokuwa nayo aliposikia Yesu anakuja kupitia njia ile. Alikimbia akatangulia mbele mahali ambapo angeweza kuwaona umati wa watu.

Lakini hakuweza kumwona Yesu pamoja na jitihada zote alizozifanya. Maana Zakayo alikuwa ni mfupi sana na watu walikuwa wakimchukia, aliwasukuma watu alipokuwa akijitahidi kupita katikati ya umati wa watu. Na hatimaye alifikiria ajaribu njia nyingine.

42.3 Kwa hiyo akakimbia akitangulia mbele ya umati wa watu, kuona kama ataweza kupata kitu ambacho kimeinuka aweze kusimama juu yake ili aweze kuona vichwa vya watu



waliokuwa wamemzunguka Yesu na pia amwone Yesu. Ndipo akapanda juu ya mkuyu uliokuwa kando ya njia ile. Matawi yake hayakuwa mbali sana, hivyo akawa amesimama juu ya tawi ambalo lilikuwa ni la kwanza kutoka kwenye shina la mkuyu. Na tawi la pili lilikuwa ni zuri kwake maana lilikuwa na majani mengi ambayo yaliyosababisha watu wasimwone. Yeye aliweza kuona kila kitu kwa urahisi; lakini kwa ajili ya majani watu wasingeweza kumwona yeye.

42.4 Mkutano ukakaribia mahali alipokuwa, kweli, Yesu alikuwepo. Hebu fikiria uso wake Zakayo ulivyofurahi. Kisha umti ule wa watu ukawa unapita ule mkuyu, Yesu akatazama juu akamwambia, "Zakayo, shuka upesi, kwa kuwa leo imenipasa kushinda nyumbani mwako." Ni furaha kubwa iliyoje kwa ajili ya mtu mfupi na mtoza ushuru! Zakayo alishuka chini na kamkaribisha Yesu kwa furaha pamoja na wanafunzi wake nyumbani kwake.

42.5 Wakati alipomwona Yesu ameingia ndani na akiwa amekaa kwenye kiti alianza kuhangaika moyoni mwake kama Yesu alimfahamu kuwa yeye ni mtu wa tabia gani. Yesu alikuwa ni mtu mwenye huruma na kwa hiyo alitaka Yesu amfikirie mema yeye pia. Hili lilimfanya ahangaike sana kwa kuwa alikuwa ni mchoyo na alipata pesa kwa watu kwa udanganyifu.

Hatimaye akaamua moyoni mwake kuweka wazi makosa yake yote aliyoyafanya. Akamwambia Yesu, "Bwana, nitawapatia nusu ya mali yangu masikini, na ikiwa nimemnyang'anya mtu kitu kwa hila nitamrudishia mara nne." Ndipo Zakayo akahisi furaha moyoni mwake alipokwisha sema hili. Lakini alikuwa na furaha zaidi alipotambua kuwa Yesu alipendezwa naye.